

ORODHA KAGUZI YA KUJISAJILI KWA WANAFUNZI WAPYA NA WANAORUDI

KUMBUKA: Wanafunzi wote wa sasa wa darasa la 8 katika Shule za Umma za Providence watapewa fomu mahususi za kuchagua shule. Fomu hizi lazima ziwasilishwe katika shule ya sasa ya mtoto kabla ya tarehe 12 Februari, 2023.

Tunatazamia kumkaribisha mtoto wako darasani. Usajili unahusisha hatua chache rahisi. Tafadhali kumbuka kwamba usajili unahitaji mzazi au mlezi wa mwanafunzi atembelee Kituo cha Usajili na Uwekaji wa Wanafunzi ana kwa ana. (Mtoto haahitaji kuwepo).

Kusanya hati zinazohitajika (za asili au zilizothibitishwa):

UTHIBITISHO WA ULEZI

- Uthibitisho wa utambulisho wa mzazi/mlezi (utambulisho wa picha) na mojawapo ya:
- Cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi kinachomtambulisha mzazi huyo huyo;
- Hati ya mahakama/kisheria inayothibitisha ulezi;
- Barua iliyothibitishwa kutoka kwa mzazi kwenye cheti cha kuzaliwa kinachomtambulisha mlezi

UTHIBITISHO MMOJA WA UTAMBULISHO WA MWANAFUNZI

- Cheti Halisi cha Kuzaliwa;
- Pasipoti;
- Karatasi za uraia;
- Kadi ya Kuwasili ya I-94; au
- Kadi ya Mkazi wa Kudumu.

UTHIBITISHO MMOJA WA UKAAJI unaoonyesha jina la mzazi/mlezi na kuwekwa tarehe ndani ya siku 60 zilizopita

- Taarifa ya upangishaji au rehani;
- Mkataba wa Kifungu cha 8;
- Bili ya gesi, umeme au simu; au
- Hati ya mshahara au taarifa ya benki.

Ikiwa iliyotajwa hapo juu haipatikani:

- Hati ya Kiapo Iliyothibitishwa ya Anwani ya Makazi–inapatikana kwenye tovuti yetu au katika Kituo cha Usajili wa Wanafunzi na uthibitisho wa ukaaji ulio na jina la mtu unayeishi naye na ambaye ameorodheshwa kwenye hati ya kiapo.

UTHIBITISHO WA CHANJO

- Uthibitisho wa chanjo/uchunguzi wa afya unaohitajika

Wanafunzi ambao wamehudhuria shule hapo awali:

- Madarasa ya K–8: Kadi ya ripoti ya hivi karibuni
- Madarasa ya 9–12: Nakala rasmi iliyo na kozi na alama
- Wanafunzi ambao wamepata huduma za Elimu Maalum za aina yoyote: Nakala ya IEP (Mpango wa Elimu Mahususi)



ILI KUJISAJILI


Tembelea www.providenceschools.org/registration.

Unaweza kujisajili kwa

1. Kuwasilisha usajili wa mapema mtandaoni kupitia ukurasa wetu wa usajili. Utakumbushwa kupakia hati zote zinazotakikana.
2. Tutumie barua pepe yenye hati na fomu zote zinazotakikana kwa info@ppsd.org
3. Pakua fomu zote, zijaze na uzilete pamoja na hati zote zinazotakikana kwa 325 Ocean St, Providence, RI 02905

HATUA ZINAZOFUATA

Ikiwa usajili umekamilika, na tathmini ya lugha haihitajiki, mzazi ataulizwa shule anayopendelea. Ikiwa utafiti wa lugha ya nyumbani unaoonyesha kwamba tathmini ya lugha inahitajika, miadi itawekwa ili mtoto akutane na mwalimu wa ESL kwa ajili ya kutathminiwa. Baada ya tathmini na uamuzi wa programu ya elimu, mzazi/mlezi ataulizwa shule anayopendelea kwa ajili ya mtoto.



SHULE ZA UMMA ZA PROVIDENCE WASIFU WA SHULE ZA SEKONDARI 2022

Kituo cha Usajili cha Wanafunzi

325 Ocean Street, Providence, RI, 02905

Simu: 456-9297 Faksi: 278-0553

www.providenceschools.org

**Providence
Schools**

SHULE ZA SEKONDARI 2022 Madarasa ya 9-12			Uandikishaji	Nyakati za Kengele	Kiwango cha Kuhitimu	Mipango ya Nje ya Shule	Riadha	Mipango ya Mtaala Ziada	Mipango ya Elimu ya Kazi na Ufundi (CTE)	Masomo na Mipango Maalum <i>Shule zote zinatoa ESL jumuisi. Mipango yote inategemea uandikishaji na ufadhili.</i>
1	360 High School 182 Thurbers Ave. (02905) Mwalimu Mkuu: Kerry Tuttlebee Naibu Mwalimu Mkuu: Richlieu Norris	(401) 274-4603 providenceschools.org/ 360	350	Saa moja na dakika hamsini asubuhi hadi saa nane na dakika thelathini na tano alasiri (7:50 a.m -2:35 p.m)	69.4%	Mipango ya baada ya shule pekee	Kwa kushirikiana na JSEC: Besiboli, Mpira wa Kikapu, Mbio za Nyikani, Kandanda, Riadha ya Ndani, Riadha ya Nje, Softiboli, Tenisi, Voliboli, Mieleka	Mtandao wa Kozi Yote (ACN), Usimbaji, Sanaa, Gentleman's Academy, Mapishi, Klabu ya Mazoezi, Mpira wa Kikapu wa Asubuhi		<ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa elimu maalum Shule ndogo ya upili iliyoungwa na wanafunzi, familia, wafanyakazi na wanajumuiya Programu inayolenga watengenezaji na Mafunzo Yanayotegemea Mradi Ushauri wa kila siku wa usaidizi wa kimasomo na ujenzi wa timu na kikundi kidogo Kozi za chuo za uandikishaji wa mara mbili na uandikishaji wa mapema Uzoeifu wa ulimwengu halisi ndani na nje ya shule Fursa za uongozi wa wanafunzi
2	Dr. Jorge ALVAREZ High School 375 Adelaide Avenue (02907) Mwalimu Mkuu: Nathan Biah Naibu Walimu Wakuu: Judy D'Antuono, Robin Mathis	(401) 456-0676 providenceschools.org/ alvarez	737	Saa mbili na dakika hamsini asubuhi hadi saa tisa na dakika thelathini na tano alasiri (8:50 a.m -3:35 p.m)	66.8%	Mipango ya kabla na baada ya shule	Kupitia mpango wa riadha wa ushirika na Mount Pleasant HS	<ul style="list-style-type: none"> All Course Network (ACN) Michezo ya Klabu Baraza la Wanafunzi Kitabu cha Mwaka 	<ul style="list-style-type: none"> CTE: Sayansi ya Kompyuta/CS4RI CTE: CNA (Uuguzi) CTE: EMT CTE: Mhudumu wa Afya ya Jumuiya 	<ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa elimu maalum Mipango wa mtoto wa kipekee Kozi za Urejeshaji wa Alama Fursa za Chuo cha Mapema Uanagenzi na Ushauri
3	CENTRAL High School 70 Fricker Street (02903) Mwalimu Mkuu: Robert Dimuccio Naibu Walimu Wakuu: Michaela Keegan, Renee Walker	(401) 456-9111 providenceschools.org/ central	1,200	Saa moja na dakika hamsini na tano asubuhi hadi saa nane na dakika arobaini alasiri (7:55 a.m -2:40 p.m)	72.4%	Mipango ya kabla na baada ya shule	Besiboli, Mpira wa Kikapu, Mbio za Nyikani, Michezo Pepe, Kandanda, Riadha ya Ndani, Riadha ya Nje, Soka, Softiboli, Tenisi, Voliboli, Mieleka		<ul style="list-style-type: none"> CTE: Sheria na Usalama wa Umma CTE: Sayansi ya Kompyuta/CS4RI 	<ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa Elimu Maalum na mipango inayojitoshesheza
4	CLASSICAL High School 770 Westminster Street (02903) Mwalimu Mkuu: Scott Barr Naibu Walimu Wakuu: Brian Baldizar, Beth Ann Battay, Nicole Mathis	(401) 456-9145 (401) 456-9147 providenceschools.org/ classical	1,115	Saa moja na dakika arobaini asubuhi hadi saa nane na dakika kumi na moja alasiri (7:40 a.m -2:11 p.m)	97%	Mipango ya kabla na baada ya shule	Besiboli, Mpira wa Kikapu, Mbio za Nyikani, Mpira wa Magongo, Kandanda, Gofu, Riadha ya Ndani, Lacrosse, Riadha ya Nje, Soka, Softiboli, Timu ya Kuogelea, Tenisi, Voliboli, Mieleka	<ul style="list-style-type: none"> Sanaa Bendi Kwaya Timu ya Hisabati Jaribio Bandia National Honor Society 		<p>KUMBUKA: Classical ni shule ya mthani.</p> <ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa elimu maalum Kozi za Uwekwaji wa Juu (AP) Mipango wa Kujiandikisha Mapema
5	E-CUBED Academy (Shule ya Sekondari) 812 Branch Avenue (02904) Mwalimu Mkuu: Matthew Juda Naibu Mwalimu Mkuu: Kerry Matheson	(401) 456-0694 providenceschools.org/ E3	389	Saa mbili na dakika hamsini asubuhi hadi saa tisa na dakika thelathini na tano alasiri (8:50 a.m -3:35 p.m)	85%	Hakuna mipango ya nje ya shule	Kupitia mpango wa riadha wa ushirika na Hope HS	<ul style="list-style-type: none"> Usimbaji Timu ya Mjadala Klabu ya Uigizaji Maandalizi ya SAT Baraza la Wanafunzi Kitabu cha Mwaka 	<ul style="list-style-type: none"> CTE: Teknolojia ya Habari ya P-TECH CTE: Mtaalamu wa Usaidizi wa Kompyuta wa IT CTE: Mitandao ya IT 	<p>KUMBUKA: E-Cubed ni shule ya maombi kwa wanafunzi wapya wanaoingia</p> <ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji/nyenzo ya elimu maalum Jumuiya ndogo ya kujifunza iliyoungwa na walimu, wanafunzi na wazazi Kozi za Urejeshaji wa Alama Fursa za Chuo cha Mapema Lugha ya Kigeni: Kifaransa na Kihispania Uanagenzi na Ushauri Sanaa ya Picha
6	HOPE High School 324 Hope Street (02906) Mwalimu Mkuu: Francisco Velasquez Naibu Walimu Wakuu: Dina Cera, Dan Geraghty	(401) 456-9161 providenceschools.org/ hope	949	Saa mbili na dakika hamsini asubuhi hadi saa tisa na dakika thelathini na tano alasiri (8:50 a.m -3:35 p.m)	69.3%	Mipango ya kabla na baada ya shule	Besiboli, Mpira wa Kikapu, Mbio za Nyikani, Michezo Pepe, Kandanda, Riadha ya Ndani, Riadha ya Nje, Soka, Softiboli, Tenisi, Voliboli, Mieleka	<ul style="list-style-type: none"> Klabu ya Uigizaji, JROTC Maandalizi ya SAT Baraza la Wanafunzi Kitabu cha Mwaka 	<ul style="list-style-type: none"> CTE: JROTC/Jeshi CTE: Sanaa ya Picha 	<ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa Elimu Maalum, mipango inayojitoshesheza, tawahudi na mahitaji ya kipekee Kozi za Uwekwaji wa Juu (AP) Kozi za Urejeshaji wa Alama Lugha za Kigeni: Kifaransa, Kiitaliano, Kihispania Uanagenzi na Ushauri Sanaa ya Picha
7	MOUNT PLEASANT High School 434 Mt. Pleasant Avenue (02908) Mwalimu Mkuu: Tiffany Delaney Naibu Walimu Wakuu: John Barnes, Michael Marino, Vilai Or	(401) 456-9181 providenceschools.org/ mtpleasant	1161	Saa mbili na dakika hamsini asubuhi hadi saa tisa na dakika thelathini na tano alasiri (8:50 a.m -3:35 p.m)	66.9%	Mipango ya baada ya shule pekee	Besiboli, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Kikapu Jumuisi, Mbio za Nyikani, Kandanda, Riadha ya Ndani, Riadha ya Nje, Soka, Softiboli, Voliboli, Voliboli Jumuisi, Mieleka	<ul style="list-style-type: none"> Kwaya Sanaa ya Picha Maandalizi ya SAT Baraza la Wanafunzi Kitabu cha Mwaka 	<ul style="list-style-type: none"> CTE: Sayansi ya Kompyuta/CS4RI CTE: Muziki CTE: Utangulizi wa Uhandisi CTE: Teacher Academy 	<ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa Elimu Maalum, mipango inayojitoshesheza, tawahudi na mahitaji ya kipekee Kozi za Urejeshaji wa Alama Fursa za Chuo cha Mapema Uanagenzi na Ushauri
8	Providence Career & Technical Academy (PCTA) 41 Fricker Street (02903) Wakuu wa Jengo: Judy Valentine, Rebecca DelBarone Mkurugenzi wa CTE: Brett Dickens	(401) 456-9136 providenceschools.org/ pcta	671	Saa moja na dakika arobaini asubuhi hadi saa nane na dakika ishirini na tano alasiri (7:40 a.m -2:25 p.m)	95.5%	Mipango ya baada ya shule pekee	Kupitia mpango wa riadha wa ushirika na Hope HS	<ul style="list-style-type: none"> SkillsUSA Klabu ya Uigizaji Klabu ya Siha Maandalizi ya SAT Baraza la Wanafunzi Kitabu cha Mwaka 	<ul style="list-style-type: none"> CTE: Magari CTE: Biashara na Utaalamu wa Vipodozi CTE: Useremala CTE: Sanaa ya Upishi CTE: Umeme CTE: Ujenzi wa Jumla CTE: Mawasiliano ya Picha CTE: HVAC/Mabomba CTE: Kutia Weko Baharini CTE: Sanaa ya Keki CTE: Utangulizi wa Uhandisi 	<p>KUMBUKA: PCTA ni shule ya kutuma maombi</p> <ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa Elimu Maalum na mipango inayojitoshesheza Sanaa Kozi za Urejeshaji wa Alama Fursa za Mpango wa Kujiandikisha Mapema (EEP) Lugha za Kigeni: Kifaransa na Kihispania Uanagenzi na Ushauri
9	Juanita SANCHEZ High School (JSEC) 182 Thurbers Avenue (02905) Mwalimu Mkuu: Robert Rametti Naibu Mwalimu Mkuu: Ariana Testa	(401) 456-1781 providenceschools.org/ sanchez	386	Saa moja na dakika hamsini asubuhi hadi saa nane na dakika thelathini na tano alasiri (7:50 a.m -2:35 p.m)	87%	Mipango ya baada ya shule pekee	Besiboli, Mpira wa Kikapu, Mbio za Nyikani, Kandanda, Riadha ya Ndani, Riadha ya Nje, Softiboli, Tenisi, Voliboli, Mieleka	<ul style="list-style-type: none"> Miradi ya Kuboresha Jumuiya National Honor Society Maandalizi ya SAT Gazeti la Shule Mabalozzi wa Wanafunzi Baraza la Wanafunzi Kitabu cha Mwaka 	<ul style="list-style-type: none"> CTE: Bioteknolojia/Matibabu CTE: Sayansi ya Kompyuta 	<p>KUMBUKA: JSEC ni shule ya kutuma maombi kwa wanafunzi wapya wanaoingia</p> <ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa Elimu Maalum na mipango ya mahitaji ya kipekee. Fursa za Chuo cha Mapema: Madarasa ya uandikishaji mara mbili na kwa wakati mmoja Kozi za Uwekwaji wa Juu (AP) Muundo wa kufundisha pamoja na Mafunzo yanayotegemea mradi Kozi za Urejeshaji wa Alama Lugha ya Kigeni: Kihispania Uanagenzi na Ushauri Sanaa ya Picha
10	TIMES² STEM Academy (MKATABA WA UMMA) 50 Fillmore St. (02908) Mwalimu Mkuu: Jensnifer Aguiar, Peter Shaughnessy	(401) 272-5094 times2.org	325	Saa mbili asubuhi hadi saa nane na dakika arobaini na tano alasiri (8:00 a.m -2:45 p.m)	85.7%	Mipango ya baada ya shule pekee	Besiboli, Mpira wa Kikapu, Gofu, Soka, Riadha, Voliboli	<ul style="list-style-type: none"> Soka ya Wavulana na Wasichana Klabu ya Sataranji Jaribio Bandia Baraza la Wanafunzi Voliboli Kitabu cha Mwaka 		<ul style="list-style-type: none"> Ujumuishaji wa Elimu Maalum